IHAIDI AFRIKA

1)Uliahidi kaka yangu,kulilinda bara langu
Waumiza moyo wangu,kuiacha nchi yangu
Uwapi utu wangu,siwaoni ndugu zangu
Iwapi ahadi yako,kulinda wadogo zako ?

2)Niliahidi kaka yako,kulilinda bara letu
Sina nguvu ndugu yako,shida viongozi wetu
Wameficha utu wako,hilo tatizo letu
Ahadi nakuahidi,kulilinda bara letu.

3)kaka yangu kila siku,ahadi ni zilezile
Huku kwetu ni usiku,tena mambo yale yale
hadi zako za masiku,majuzi na tangu kale
nimechoka yako ahadi,kulilinda bara letu

4)Huku kwetu mbona shida,tunayo demoghasia
Umeshapotea muda,watu wanaangamia
vichenchi vile vya soda,ndivyo wanadanganyia
Kaka yangu sema kweli,kama bara walipenda

5)Nilitambua mengi sana,ndo maana nikakimbia
Nilitaka kuungana,muda ulishapotea
Nyumbani tunashidana,na hatuna mazoea
Hakuna demokrasia,kwao ni demobandia.

6)kaka yangu nakuita,sikia kilio changu
Chozi langu lishakata,moyoni nauchungu
Ni nani wakulifuta,siwaoni ndugu zangu
Ahadi ya bara hili,ni kuzidisha uchungu.

7)hii ni ahadi yangu,kesho narudi nyumbani
Kulijenga bara langu,liwe kama la zamani
Tusiwe tena mafungu,irudi yetu Amani
Hii ni ahadi yangu,kulilinda bara langu.

8)ona kaka huku shida,tunavyopigwa mabomu
Wao wanatoa oda,tuchinjwe hata kwa sumu
Huku wamepaka poda,wenyewe twajilaumu
Afrika hii ya leo,si kama ile ya jana

9)hatuna tena upendo,zamani ulipotea
Tumezidisha magendo,na chuki twaimezea
Udugu twatupa kando,kiama twakingojea
Kama mwisho wa dunia,ni hapa utaanzia

10)Kaka timiza ahadi,bara linateketea
Onyesha yako juhudi,kabla hatuja potea
Hiyo ndo yetu ahadi,utakayo tulete
Tuaahidi waafrika,Amani watulindia.

SHAIRI-IHAIDI AFRIKA
MTUNZI-Idd Ninga wa Tengeru Arusha
+255624010160
iddyallyninga@gmail.com